# Wizara ya Elimu nchini Amerika
# Idara ya Haki za Kiraia:

---

# Ithibati ya Elimu bora ya Hali ya Juu kwa Wote

U.S. Department of Education
Office for Civil Rights
Washington, DC 20202-1100

**Marekebisho Septemba 2004**

## Umuhimu wa Sheria za Haki za Kiraia

Utekelezaji sheria za Haki za Kiraia za Marekani ni jambo lililo saidia kuleta mabadiliko makubwa sana katika mfumo wa elimu wa Marekani na kuboresha utaratibu wa kielimu kwa mamilioni ya wanafunzi. Vizuizi vingi ambavyo viliwazuia wengi kuweza kujichagulia huria elimu na taaluma za kazi walizo penda kufanya, vimeondolewa. Hivi sasa, taratibu nyingi za shule, zinawapa nafasi hata wanafunzi wasioweza kuongea lugha ya Kiingereza kwa ufasaha katika mipango yao ya elimu. Wanafunzi wengi zaidi walemavu, wanaweza sasa, kwa utumizi wa huduma mbali-mbali na vifaa vya kuwasaidia kushiriki madarasa ya kawaida.

Pamoja na hayo, Sheria ya Haki ya mtoto ya mwaka wa 2001 (No Child Left Behind Act of 2001) (NCLB), sheria inayoleta pamoja uwiano wa utaratibu wa mipango ya elimu nchini Amerika, inaimarisha jukumu la Wizara la kuhakikisha nafasi sawa ya elimu kwa wote na kuimarisha ubora wa elimo kote nchini. Sheria ya (NCLB), ina vipengele vinavyo shinikiza kuwa watoto wote wana haki ya kupata elimu bora bila ya kujali kabila, ukoo, jinsia, ulemavu au hali yao ya kijamii ya mtoto.

Sheria za Haki za Kiraia zilifungua milango ya shule zetu, madarasa na vyuo, viwanja vya riadha na kumbi nyingine. Kama matokeo, watu wa Marekani ambao wanatoka nchi na tamaduni tofauti wamepitia milango hiyo ya elimu kwa ufanisi, kiasi kwamba, baadhi wameonyesha vipaji vya kuwa viongozi wa baadaye wa taifa la Marekani katika fani ya kibiashara, kiutawala, kisayansi, kisanii na hata kielimu. Sheria za Haki za Kiraia zimeambatanishwa na Sheria ya Haki za Mtoto (NCLB) ili kuhakikisha kuwa milango hiyo ya elimu itasalia kuwa wazi kwa wote.

## Majukumu ya Idara ya Haki za Kiraia

Idara ya Haki za Kiraia (OCR), iliyo katika Wizara ya Elimu, ni taasisi inayo husika na utekelezaji wa sheria za Shirikisho na kuhakikisha kuwa taasisi za elimu zinazo pokea ufadhili wa kifedha wa serikali ya Shirikisho hazijihusishi hata kidogo na kashfa ya ubaguzi. OCR iliyo katika (U.S. Department of Education) na (Wizara) inashinikiza sheria za Shirikisho za Haki za Kiraia zinazo piga marufuku ubaguzi kwa misingi ya kabila, rangi, asili ya mtu, jinsia, ulemavu na umri katika ratiba na shughuli zinazo pokea ufadhili wa fedha kutoka Wizara ya Elimu. Sheria za haki za kiraia ndiyo dhamana ya kitaifa kwa minajili ya kufuta ubaguzi katika mfumo wa elimu na shughuli nyingine. Sheria hizo ni;

- Ibara ya VI ya Haki za Kiraia ya 1964 (Civil Rights Act of 1964) (inapiga marufuku ubaguzi kwa misingi ya kabila, rangi, asili ya mtu);

- Ibara ya IX ya Sheria iliyo rekebishwa ya mfumo wa Elimu ya 1972 (Education Amendments of 1972) (inapiga marufuku ubaguzi kwa misingi ya kijinsia);

- Fungu la 504 lililo durusiwa la Hadhi ya utu la 1973 (Rehabilitation Act of 1973) (linapiga marufuku ubaguzi kwa misingi ya ulemavu);

- Sheria dhidi ya ubaguzi kwa misingi ya Umri ya 1975 (Age Descrimination Act of 1975) (inapiga marufuku ubaguzi kwa misingi ya umri wa mtu); na

- Ibara ya II ya sheria kuhusu Wamarekani Walemavu ya 1990 (Americans with Disabilities Act of 1990) (inapiga marufuku kubaguliwa walemavu katika taasisi za serikali, ikiwa ni pamoja na shule za wilaya, koleji za serikali na vyuo vikuu, shule za umma za ufundi wa kazi na maktaba za umma iwapo taasisi hizo zinapokea au la ufadhili wa kifedha).

Pamoja na hayo, OCR inatumia Sheria ya Haki za Boy Skauti wa Marekani ambayo ni sehemu ya Sheria ya Haki za Mtoto ya 2001. Chini ya sheria inayo mlinda Boy Skauti wa Marekani, hakuna kituo cha elimu ya msingi cha serikali, shule ya upili ya serikali au vituo vingine vya elimu vinavyo weza kuwakatalia kukutana akiwa mmoja au wengi Boy Skauti katika nyenzo za taasisi hizo kabla au baada ya shule au kubaguliwa, na kundi jingine lolote lile lililo na uhusiano na Boy Skauti wa Marekani, au kundi lolote la vijana lililo orodheshwa katika Ibara ya 36 ya sheria za Shirikisho la Marekani kama sheria ya uraia mwema

Jumla ya harakati za OCR ni kujihusisha na utekelezwaji sheria katika afisi zote kote nchini. Mjini Washington D.C. Afisi ya Msaidizi wa Waziri wa Haki za Kiraia ndiyo inayo husika na uongozi na mawasiliano fani ya utekelezwaji sheria hizo.

**Sheria hizo zinatekelezwa katika taasisi za Elimu**

Sheria za Haki za Kiraia zimeenezwa katika taasisi zote za kielimu kitaifa. Hii ni tangu taasisi zote za Elimu zimekuwa zikipewa msaada wa kifedha na serikali ya Shirikisho. Hii ikiwa na maana lazima ziheshimiwe sheria za haki za kiraia:

- kiasi cha shule 15,000 za wilaya;

- zaidi ya koleji na vyuo vikuu 4,100;

- kiasi cha taasisi 5,000 zinazo toa vyeti vilivyo chini ya kiwango ch shahada, kama vile shule za taaluma za uendeshasji magari, na wafanyao kazi masaluni na:

- na maelfu ya taasisi nyingine kama vile maktaba, majengo ya ukumbusho wa kale, shule za ufundi wa kazi, na vituo vya marekebisho ya tabia.

**Sheria hizo zinatekelezwa kwa Wanafunzi na Wafanyakazi**

Sheria za haki za kiraia zinawapa fursa idadi kubwa ya wanafunzi kusoma, au kuomba kusoma katika taasisi zetu za elimu, kama ifuatavyo:

- kiasi cha wanafunzi milioni 54.3 wanao soma shule za msingi na za upili, na

- kiasi cha wanafunzi milioni 16.4 wanao soma katika koleji na vyuo vyetu vikuuabout

Katika baadhi ya matokeo sheria hizo zinawapa fursa wanao fanya kaz, kuomba ajira katika taasisi za elimu.

**OCR hupokea Malamiko dhidi ya Ubaguzi kutoka Raia wa Kawaida**

Njia moja muhimu ni kuwa OCR hubeba jukumu la kutatua malalamiko yaliyo failiwa na wanafunzi, wazazi na watu wengine. Mtu au shirika lililo toa malalamiko hakuna haja ya kuhusika binafsi na madai ya kubaguliwa, bali yawezekana kufanya hivyo kwa niaba mtu mungine au shirika. Kwa jumla OCR yaweza kufanya jambo katika kujali malalamiko endapo malalamiko yalifailiwa katika muda wa kalenda wa siku 180 tangu kilipo tokea kisa cha madai ya ubaguzi, au malalamiko yanayo dai kuendelea vitendo vya ubaguzi.

OCR hupokea kwa wastan malalamiko 5,000 kila mwaka. Malalamiko hayo huwa yanahusika hasa na maswala ya haki ya elimu bora kwa wote.

Chini ya Ibara ya VI — malalamiko kuhusu — kabila, rangi, asili ya mtu huwa na maswala kama vile:

- watu kutengwa kwa misingi ya kikabila na kiukoo ikiwa ni pamoja na uwezo wa kundi husika;
- watu kutengwa katika huduma ya lugha nyingine kwa wajifunzao lugha ya Kiingereza;
- Visa vya kulazimishwa nidhamu;
- Wanafunzi kuamrishwa sera fulani, ikiwa ni pamoja na kutunukiwa zawadi na wengine kuwekwa katika makundi ya wenye vipaji;
- Kupewa uhamisho baina ya wilaya;
- Kutotenganishwa katika shule;
- Unyanyasaji wa kikabila;
- Malasi ya wanafunzi katika mabweni ya kolejina vyuo vikuu; na
- Vyeo vya kielimu.

Chini ya Ibara ya IX — malalamiko ya ubaguzi wa kijinsi huwa kuna maswala kama:

- unyanyasaji wa kijinsia;

- mlingano wa haki ya elimu viwango mbali mbali na upande wa michezo;

- huduma kwa wanafunziu walio shika mimba; na

- kuruhusiwa vyuo vikuu baada ya elimu ya sekondaria.

Chini ya Fungu la 504 na Ibara ya II — malalamiko ya ubaguzi dhidi ya ulemavu huwa mna maswala kama:

- kuruhusiwa katika shule na nyenzo zake pamoja na ratiba;

- mfumo wa huduma maalumu wa elimu;

- tathmini na kupasndishwa wanafunzi wanao hitaji huduma maalumu ya kielimu;

- wanafunzi kusomeshwa katika mazingira maalumu kufuatana na mahitaji yao ya kielimu;

- kusimamishwa na hata kufukuzwa kwa wanafunzi walemavu;

- kutambua kiwango cha elimu na marekebisho pamoja; na

- misaada ya ziada kwa wanafunzi walio na matatizo ya kusikia, wasio weza kufanya lolote kwa mikono au wasio na ujuzi wa kusema.

**OCR hutatua vipi Malalamiko**

Malengo ya msingi ya OCR fani ya utatuzi wa malalamiko, ni kutatua mara moja madai ya ubaguzi kwa njia ya haki na kikamilifu. OCR iligundua kuwa njia bora zaidi kama jawabu la matatizo ni ushirikiano baina ya wanafunzi, wazazi, jumuia ya watu, serikali na taasisi za elimu, shule na koleji.

OCR hutumia njia mbali mbali ili kutanzua malalamiko, kuanzia kufanya uchunguzi wa malalamiko, kuzungumza na wahusika ili wahiyari kuafikiana.

Ni baada tu ya OCR kugundua ya kwamba watu wameshindwa kuhiyari kuelewana ndipo OCR itachukuwa hatua za kiutawala kwa kusikiliza wahusika au ipeleke kesi kwa Wizara ya Sheria. Utaratibu huo huiwezesha OCR:

- kuingilia kwa wakati mwanzo wa matatizo ya malalamiko;

- kutafuta muafaka dhidi ya hali yoyote ile ya ubaguzi; na

- kuwasaidia wanafuzi, wazazi na viongozi wa shule kupata jawabu la malalamiko.

**OCR hufanya Tathmini ya Muafaka**

Taasisi hiyo huanzisha kesi inayoitwa tu “tathmini ya muafaka,” inayo iwezesha OCR kuelewa misingi ya matatizo yaliyo jitokeza, iwapo ni matatizo yaliyo kutwa au ni matatizo mapya yaliyo jitokeza.

Kufahamu hali kamili ya maelewano ni jambo linalo isaidia OCR kusawazisha na kutekeleza wajibu wake. Lengo la Tathmini ya Maelewano ni kuhakikisha kuwa makundi ya wasio jiweza mathalani masikini dhalili au wasio weza kujieleza katika lugha ya Kiingereza, na ambao pengine hawajui sheria haki zao za kiraia zinalindwa. Uzoefu wa OCR unaonyesha kuwa kujihusisha makini na tathmini za maelewano daima ni jambo linalo fanya walio husika katika mkwaruzano kutoa mapendekezo yanayo tokea kuwa sera au kuwa mipango vinavyo wasaidia idadikubwa ya wanafunzi — kiasi kwamba, na hata baadhi ya malalamiko ambayo bado hayajajitokeza hupata baadhi ya majawabu.

OCR huchagua baadhi ya tathmini za muafaka kutokana na chemchem mbali mbali za maelezo zilizo hifadhiwa kwa misingi ya maelezo yaliyo tekelezwa na walalamikaji, taasisi za elimu, vyombo vya habari na raia wa kawaida. OCR hufanya tathmini ya katika maswala kama:

- wanafunzi wachache katika kitengo maalumu cha elimu na viwango vya chini;

- Wajifunzao Kiingereza kuweza kuzungumza katika lugha nyingine wanayo dhibiti ili kunufaika na ratiba zote za kielimu;

- Elimu bure katika vituo vya shule za umma kwa wanafunzi walemavu;

- Wanafunzi wachache kupewa zawadi kwa vipaji vyao na kuwaweka madarasa ya juu kutokana na uwezo wao;

- Mateso ya rangi;

- Mandhari ya shindani kimwili; na

- Maungamano katika chuo kikuu, shule ya msingi na pia chou cha secondari.

OCR inatambua kwamba serekali, mawakili ya elimu, wazazi na pia watu wanaosisitiza wote wanashirikiana mradi moja ya kupatia hatua yanayolingana na pia kuwakubalisha mifao ya elimu. OCR inaunganisha ustadi wa shiriki zao pamoja na washika dau, ili itoe mitambulifu yalioyofaidia, kama unganguzi ya elimu yanayo ongeza hatua za wanafunzi wote.

**Huduma ya istlahi ya OCR inasaidia watu na Jumuiya**

Maazimio ya huduma ya Istlahi ya OCR inazuia uhalifu wa sheria ya Haki za kiraia. Hi inawezekana kwa kasaidia wapokeaji wafuate sheria na kusaidia waliyofaidia kuelewa haki zao. Kuna wanafunzi millioni wanaohifadhiwa na sheria ya Haki za Kiraia, OCR ikiwa pekeyake, inajua kwamba haiwezi kusimamisha ubaguzi isiyokubalishwa katika elimu. Kwa hiyo ni lazima Wanfunzi,wazazi na walime wakue na elime na ujuzi ili wahakikishe kwamba ubaguzi isiyokubalishwa isikafanyike.

OCR inapatiana huduma kuhakikisha utimulifu wa majumuia katika wakati wa uimarisho ya mashtaka au katika marudio ya utumilifu. Pia OCR ina orodha kubwa ya kupatiana huduma ya istlahi kama mkutano ya kuonana, madarasa ya kufundisha,mukutano na ushirikiano kwenye muktano. Pia OCR inajibu maswali na inaomba usaidizi kutoka mawakili za federali, za serekali, za elimu ,wazazi,wanafunzi na wanainchi.

Inaidara nyingi za OCR zimefundisha huduma ya timu yao iwe ambilika kwa washariki wetu, washika dau na wanainchi. OCR imeanzilisha http://www.ed.gov/ocr, ambayo imeunganishwa na web ya Wizara yetu.

**Mailiko ya Mbele**

Isipokuwa kwa maendeleo yaliyoletwa na ufuataji wa sheria ya haki za kiraia, bado kuna watu katika taifa wanaokatazwa hatua za elimu. Bado Kuna sera na vitendo vinavyokataza mikundo yanayoalika na miradi kwa vilema, wanawake, wamerikani wazee. Utazamaji kwenye mradi wa utumilifu wa haki za kiraia — mpenyepenye ya kifano, ubora wa elimu, na wastani wa juu kwa wanafunzi wote — ni uwekezaji utakaofanywa kama tunataka hali ya baadaye ya Amerika iwe thabiti.

**Hakiikisho Kwa OCR**

Timu ya Huduma kwa Wateja katika makao makuu ya taifa ya OCR, inajibu maswali kwa simuya dharura ya OCR. Watu wanatumia simu hii kuuliza juu ya maswala mbali-mbali juu ya sheria za haki za kiraia na pia sera za OCR na maelekezo, na pia maelezo kuhusu miradi yetu ya OCR.

Ukitaka habari kuhusu sheria za haki za kiraia, au maana ya kutekeleza ukamili wa haki za kiraia, au kupewa usaidizi, unaweza kuwasiliana na maafisa wa idara iliyokatika eneo lako. Idara inaweza kupatikana katika:
http://www.ed.gov/ocr/contactus.html.

Ukitaka maelezo mengine zaidi:

**Simu Ya Dharura ya OCR ni:**
1-800-421-3481;TDD: 877-521-2172

**Barua Pepesi:** OCR@ed.gov

**Mtandao:** http://www.ed.gov/ocr